GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWAW TE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. 237 **MUHAR-SAFAR** 1445 **AH** **SEPTEMBA** 2023 **ZAHOOR** 1402 **HS** **BEI TSH 800/=**

Jalsa Salana Uingereza 2023

Kilele cha Mafanikio Zaidi

'Mtazamo wa Baraka za Mkusanyiko wa Ajabu wa Kiroho wa Waumini'

Baada ya kusoma Tashahhud, Ta'awwuz na Surah Al-Fatihah, Khalifa mtukufu, Hazrat Mirza Masroor Ahmad (atba) alisema kwamba shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu. Mwishoni mwa wiki iliyopita, kwa neema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mkutano wa Mwaka (Jalsa Salana) wa Uingereza ulifanyika kwa mafanikio. Licha ya hali ya hewa wakati fulani kuchukua mwelekeo mbaya, shughuli zote kwa ujumla ziliendelea vizuri. Vivyo hivyo, mahudhurio yalikuwa makubwa zaidi kuliko miaka iliyopita.

Baraka Tulizomiminiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu Katika Jalsa Salana hii

Khalifa mtukufu (atba) alisema

...Ukurasa.5



Hadhrat Ameerul Mumineen Hazrats Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih Wa tano[atba] akihutubia waumini katika Msikiti wa Baitul Futuh, Morden, London, Uingereza – Siku ya tarehe 04 Agosti 2023.

Jalsa Salana Kanda ya Ziwa yanoga

HABARI UK> 3

Na.
Maulana Sheikh Shaban A. Shunda

Mwaka huu, 2023, Jumuiya ya waislam waahmadiyya katika kanda ya ziwa ilifanya Jalsa Salana ya kanda mjini Kagongwa, manispaa ya Kahama. Mkutano huo ulifanyika katika ukumbi wa Poneka (Poneka Hall) Kagongwa. Ulikuwa ni mkutano wa siku mbili uliofanyika tarehe 5-6, Julai, 2023. Wanajumuiya takriban 1300 kutoka katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Mwanza, Simiyu na Tabora walishiriki katika mkutano huo. Amir Sahib akiwa na ujumbe wake kutoka makao makuu alishiriki mkutano huo akiwa katika ziara yake ya kanda ya ziwa. Viongozi wakuu wa Tanzim za Lajna na Amsarullah pia walishiriki katika mkutano huo wakiwa na baadhi ya wajumbe wa majlis amla zao. Sadr wa Majlis Khudamul Ahmadiyya aliwakilishwa na wajumbe wawili wa Majlis Amla kutoka makao makuu, walioungana na Naib Sadr wa kanda ya ziwa Bw. Abdallah Mgunya.

Ufunguzi wa Maji na Msikiti (Humanity First na IAAAE)

Mhe. Amir na Mbashiri Mkuu, Tahir Mahmood Chaudhry Sahibalifungua rasmi Msikiti mpya Masjid Baitul Wasey na kisima cha maji katika eneo la Kagongwa mkoani Shinyanga) katika ziara yake ya kanda ya Ziwa,



Yesu aliongozwa na nani Nyikani?

Bwana Hassan Mkwahe – Masasi

Injili ya Mathayo katika sura ya nne imeanza kwa maneno yasemayo:-

«Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi.

Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa.

Majaribu akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe

HABARI UK> 4

>UK .4 Yesu aliongozwa na nani Nyikani?

Ziara ya Prof. Abdul Salaam, BENIN >UK .8

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Jalsa Salana ya Uingereza ya Julai 28,29,30

Mazungumzo. Hali ya hewa. Vyombo vya habari. Usafiri huko hadi kule katika jiji la London yote hayo kwa ujumla yalitawaliwa na maneno matatu *Jalsa Salana Uingereza*. Watu walioomba likizo ili wapate fursa ya kuwahudumia wageni wa Nabii wa Allah. Masih Aliyeahidiwa[as]. Usiku na mchana, wanapanga, wanarekebisha ili mradi wakamilishe kwa ufanisi majukumu waliopewa. Kazi hii wanaikamilisha kwa ubora wa hali ya juu. Matangazo yanaenea Mashariki na Magharibi kuhusu tarehe 28, 29 na 30. Julai siku za mkutano. Vipeperushi, Luninga, Radio, Vyombo vya kijamii vyote hivyo vinatumika kwa ubunifu mkubwa kuhamasisha na kuwahabarisha Binadamu kuhusu mkutano huu ambao si kama mkutano wa kidunia. Huu ni mahsusi katika kusafisha nafsi ili ifike katika nafsi yenye matumaini.

Siku zina Mabawa. Tarehe taratibu. Siku zinakaribia. Mahali pa kufikia wageni wa Masihi Aliyeahidiwa[as] ni tayari. Uwanja wa Mkutano unavutia. Vitabu vilivyochapishwa na Jamati vimewekwa palipo wazi. Ukumbi wa hisitoria ukiwa umesheheni picha unaongeza uzuri. Vyumba vya kurushia matangazo viko tayari. Kiongozi wa kiroho Hazrat Mirza Masroor Ahmad atba anakagua shughuli zote. Jikoni anazungumza na wapishi na kuonja Chakula. Anakutana kwa pamoja na wale wote wanaojitolea. Anawashukuru kwa kujitolea kwao na kuwakumbusha wajibu mkubwa walionao. Anawakumbusha waombe sana kwa Allah ili awasaidie kutimiza wajibu wao. Hakuna jambo lolote linalofanikiwa bila Baraka na Rehema za Allah. Anawataka wawe wavumilivu wakifanya yote hayo ili kupata radhi za Allah. La mwisho lakini si kwa umuhimu wakati wote kubeba TABASAMU Usoni. Tabasamu ni dawa inayomtibu anayetabasamu, ni dawa kwa yule anayekutana na Tabasamu.

Siku hazikawii. Tarehe 28 Julai Huzur anafungua Jalsa Salana akiwakumbusha shabaha ya kuanzishwa kwa Jalsa Salana ambayo ni kupata Uchamungu, kujiongezea elimu na kujenga undugu. Siku mbili zinazofuata Huzur anaelezea neema zilizoshuka katika Jamati Ahmadiyya. Hata hivyo anasisitiza kuwa hata ufanyeje huwezi kuzihesabu neema za Allah. Wajibu ni kushukuru na kushukuru zaidi. Vitabu vipya vimechapishwa. Misikiti imejengwa. Visima vinatoa maji safi, Hospitali zimejengwa. Watu wanajiunga kupitia njozi na mahubiri. Siku ya mwisho Huzur anaelezea wajibu tulionao katika kuondoa shida walizonazo Masikini katika kuwasaidia tunatimiza wajibu wetu na kutafuta mapenzi ya Allah. Wale ambao wanakodolea Mali waliyopewa watu waache kwani hicho ni chanzo kikubwa cha umasikini.

Taswira tunayopata kuhusu Jalsa Salana si nyingine isipokuwa muujiza. Watu kutoka kila pembe ya Dunia wa rangi, utamaduni dini kuwa pamoja kwa siku tatu wakiishi kwa Mapenzi na kuheshimiana, hii ni nini kama sio muujiza? Ni alama nyingine ya ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad as. Aliyepewa ahadi na Allah kuwa atafikisha ujumbe wake Kila pembe ya Dunia. Hakuna hata neno moja la ufunuo huo lililoanguka chini. Na ikumbukwe ahadi hiyo ilitolewa kwa Masih Aliyeahidiwa[as] akiwa katika kijiji kidogo cha Qadiani huko India.

Jicho la busara bila shaka litatizama na kujiuliza, nini hasa siri ya mafanikio haya? Siri ya mafanikio haya ya Jumuiya ya Ahmadiyya ni ile iliyopatikana wakati wa Ukhalifa ulioongoka wa Mtukufu Mtume Muhammad saw . Maendeleo makubwa yalipatikana kwa sababu ya kuendelea kushika kamba ya Allah ambayo ni Ukhalifa. Ni jambo la muhimu kuendelea kusisitiza tena kusisitiza kwa nguvu zote kuwa Khalifa anachaguliwa na Allah. Sote tumeshuhudia jinsi gani maombi ya Huzur yanavyopokelewa. Hiyo ndiyo siri ya mafanikio ya Jumuiya ya Ahmadiyya. Na hili tunao wajibu kulieleza kwa mapana na marefu. Maendeleo yetu, ufanisi wetu, elimu yetu, ushujaa wetu, vyote hivi ni baraka ya Ukhalifa.

Sisi tuliyopata neema hii, tunao wajibu wa kuenzi kwa mapenzi na ghera kubwa Ukhalifa. Mafanikio yetu. Uhai wetu. Elimu tuliyonayo. Sifa zote tunazomwagiwa tukumbuke, yote hayo yanatokana na Ukhalifa. Hivyo tuzidi kumuomba Allah na katu tusikubali chemchem hii ikauke. Tuendelee Inshallah tuitunze chemchem hii ili iendelee kutupatia maji ya kiroho, ambayo kila anayekunywa huondoa kiu. Chemchem hii unaweza kuifaidi kwa njia tatu. Mara kwa mara Khalifa wa Allah anatoa mwongozo wa maelekezo, tuwe wepesi wa kutekeleza maagizo hayo, kwani hiyo ndio njia ya ufaulu. Jumuiyaa ya Ahmadiyya inagawa mali na mali yenyewe ni vitabu vinavyotolewa na Jumuiya ya Ahmadiyya. Khalifatul Masih[atba] amesisitiza sana kuhusu usomaji wa vitabu. Tuweke maanani na kutekeleza wito huo na kila Ijumaa kwa msaada na huruma ya Allah tunasikiliza hotuba ya kiongozi wetu Mpendwa. Tujiwekee utaratibu wa kuhakikisha Inshallah kuwa tukisikiliza hotuba hizo. Kwa hivi sasa hakuna chimbuko la elimu kuliko maneno matakatifu yanayotolewa na Khalifa wa Allah duniani.



QUR'AN TUKUFU

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ
لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْاَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ مِنْ
قَبْلِهِمْ ۪ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِيْنَهُمُ الَّذِي ارْتَضٰى لَهُمْ
وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ اَمْنًا ؕ يَعْبُدُوْنَنِيْ
لَا يُشْرِكُوْنَ بِيْ شَيْـًٔا ؕ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ
هُمُ الْفٰسِقُوْنَ ۝٥٦

Tafsiri :
Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na chochote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri.



NUKUU YA HADITHI

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Hurairah r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Hakika kuna baadhi ya malaika watukufu wa Mwenyezi Mungu ambao wanazunguka ili kutafuta mikutano ambamo Mwenyezi Mungu anatajwa. Basi wanapokuta mkutano ambamo Mungu anakumbukwa, huwa wanakaa pamoja nao, baadhi yao wakiwafunika wenzao kwa mabawa yao hata kwamba wanajaza nafasi iliyo baina yao na baina ya mbingu ya karibu. Na watu wanapotawanyika baada ya mkutano huo, malaika wanapaa kupanda hadi mbinguni na hapo Mungu anawauliza, naye anawajua sana, ya kwamba walitokea wapi? Nao wanasema: Tumetokea kwa watumishi wako waliopo ardhini ambao walikuwa wanakutukuza na kutangaza ukubwa wako na kukuabudu, kukuhimidia na kukuomba. Mungu anasema: Wananiomba nini? Wanasema: Wanakuomba Pepo yako. Mungu anauliza: Je, wameiona Pepo yangu? Wanasema: La, E Mola. Ndipo Mungu anasema: Wangeliomba sana namna gani kama wangelikwishaiona Pepo yangu! Malaika wanasema: Nao walikuwa wanajikinga kwako. Mungu anauliza: Je, walijikinga kwangu katika nini? Wanasema: Katika Moto wako, E Mola. Anasema: je, wameuona Moto wangu? Wanasema: La. Basi Anasema: Wangejikinga sana kwangu namna gani kama wangekwishauona Moto wangu! Na malaika pia wanasema: Nao walikuwa wanakuomba ghofira. Na Mungu anasema: Nimewasamehe, basi nimewapa waliyoomba, na nimewakinga katika kile walichotaka kingwa. Hapo malaika wanasema: E Mola, lakini kati yao pia alikuwepo fulani aliye mtu mwenye makosa mengi. Huyo akapita kwao na kukaa tu nao hivi bila kutia uzito jambo hilo. Lakini Mungu anasema: Hao ndio watu ambao mwenye kukaa nao hawezi kuwa na bahati mbaya. (Muslim).



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Hazrat Khalifatul Masihi wa Tano[atba] anasema:
"Lengo ambalo kwa ajili yake tumekusanyika hapa ni lengo kubwa sana. Lengo ni kutosheleza kiu yetu ya kiroho; lengo ni kujiongezea elimu ya kidini; lengo ni kujifunza njia za kutimiza haki za Allah na za binadamu; basi kwa ajili yake angalau tunatakiwa kujitolea hisia zetu na pia kumwomba Allah msaada kwa maombi. … Hivyo, jitahidini kujaza siku hizi kwa maombi na dhikri ya Mwenyezi Mungu." (Hotuba ya Ijumaa, 5 Agosti

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Jalsa Salana Kanda ya Ziwa yanoga

Kutoka 1..

Mkutano ulifunguliwa mnamo majira ya alasiri tarehe 4, Julai, 2023. Amir Sahib alipofika katika ukumbi wa mkutano alilakiwa kwa shangwe nyingi za takbiir. Kabla ya kuingia ukumbini aliongoza zoezi la upandishaji wa bendera ya Jamaat na ile ya taifa.



Kisha aliingia ukumbini na mkutano ukafuguliwa kwa usomaji wa Kurani tukufu, iliyosomwa na rais wa tawi la Kagongwa Mwl Faris Mbaule. Kisha Amir Sahib alitoa hotuba fupi ya ufunguzi, akielezea malengo ya jalsa salana. Alisema kuwa lengo kuu la mkutano huo ni kupata elimu ya kiroho na kuwataka wahudhuriaji kutumia muda wao mkutanoni hapo kujipatia faida za kidini kwa kusikiliza hotuba mbali mbali zitakazotolewa.



Kadhalika aliwataka wahudhuriaji kutopoteza muda kwa matembezi na maongezi yasiyokuwa na faida. Badala yake aliwataka kutumia wasaa huo kufahamiana wao kwa wao, maana wametoka katika maeneo mbali mbali ya kanda ya ziwa. Aliwasisitiza wanajumuiya hao, ambao wengi wao walikuwa ni wapya kushiriki hatua zote za jalsa sawa na ratiba. Alibainisha pia ya kwamba siku hiyo hakungekuwa na ratiba ndefu ya jalsa. Bali ilitengwa rasmi kuzipa nafasi tanzimu za jamaat kukutana na kuzungumzia mikakati mbali mbali juu ya shughuli zao.

Amir Sahib aliondoka baada ya hotuba yake na kutoa nafasi kwa viongozi wa Tanzim kukutana na wanachama wao ili kujadili mambo yao ya kitanzimu. Vikao vya Tanzim viliendeshwa katika ukumbi huo huo wa mkutano. Khudamul Ahmadiyya na Ansarullah walikutana katika maeneo tofauti ndani ya ukumbi wa wanaume, huku Lajna wakiutumia ukumbi wa wanawake.

Kikao cha Khudam kiliongozwa na Naib Sadr wa kanda ya kati, Bw Abdallah Msesemele, huku kikao cha Ansarullah kikiongozwa na Sadr wa Tanzim hiyo Dk Saleh Kitabu Pazi. Lajna kwa upande wao walifanya kikao chini ya Sadr wao Bi Zena Nyange.



Katika vikao hivyo, viongozi wa tanzimu walitumia nafasi hiyo kutambulisha malengo na umuhimu wa tanzimu hizo katika jamaat. Waliwafahamisha washiriki wa mikutano hiyo juu ya nidhamu na mfumo wa uongozi katika tanzim. Pia walielezea wajibu wa kila mwana tanzim na kutoa wito kwa wana tanzimu kushiriki ipasavyo katika shughuli za kitanziim. Kwani walisema kuwa hiyo ni njia bora zaidi ya kuisaidia jamaat katika utekelezaji wa malengo yake. Viongozi hao pia walisisitiza ubunifu katika kushiriki mambo mbali mbali ya kitanzimu kama vile, mahubiri, waqar i amal, kutembelea wagonjwa na wasiojiweza. Waliagiza pia kufanyika kwa uchaguzi wa viongozi wa tanzimu katika kila tawi la jamaat. Mwishowe waliwahimiza viongozi wa tanzimu wa ngazi ya matawi kila mwezi,kutuma taarifa makao makuu, juu ya shughuli ya maendeleo ya shughuli za kitanzimu. Vikao hivyo viliendelea hadi majira ya saa 3:00 usiku



Siku ya Alhamisi, tarehe 6, Julai, mkutano ulianza majira ya saa nne asubuhi, chini ya uenyekiti wa Amir Sahib. Kurani Tukufu pamoja na tafsiri ilisomwa na MwlShukuru Suleiman Magana wa Kahama,ikifuatiwa na shairi lililosomwa na Mwl Shirazud din Hamza. Mada ya kwanza ilitolewa na Naib Amir, Sheikh Abdul Rahman Ame, ambaye alielezea muundo wa nidhamu ya Jamaat. Humo alifafanua juu ya mfumo wa uongozi katika jamaat na kusisitiza umuhimu wa utii chini ya nidhamu hiyo. Akirejea aya za Kurani Tukufu, Hadithi za Mtume saw, kauli za Masihi aliyeahidiwa na nukuu za makhalifa wake, Sheikh Ame aliwanasihi waahmadiyya wapya na wazamani juu ya kusimamisha sala na kujitolea kifedha. Aliwasihi waahmadiyya wapya kwamba angalau wanaweza kujizoeza na nidhamu ya kujitolea kifedha kwa kuanza kushiriki michango ya ahadi kama vile Tahrik jadid na Wakfu Jadid.



Mada ya pili ilitolewa na Maib Amir wa pili, Sheikh Abid Mahmoud Butt, ambaye alihutubu juu ya ujaji wa Masihi na Mahdi. Sheikh huyo, ambaye pia ni mkuu wa Chuo cha Jamia Ahmadiyya Morogoro, alianza hotuba yake kwa kuelezea bishara mbali mbali juu ya ujio wa mkombozi mmoja katika zama za mwisho, zilizomo katika dini mbalimbali.

Alitoa mifano ya dini za uhindu, uyahudi, ubudha, ukristo na hata Islam, kwamba zote zimebashiri juu ya ujio wa mwokozi wa kiroho kwa wanadamu katika zama za mwisho. Kisha akatoa ufafanuzi uliofanywa na Mtume saw juu ya bishara zote zihusuzo ujio wa mara ya pili wa waanzilishi wa dini. Alielezea bishara ya Mtume saw juu ya kusawijika kwa hali ya kiroho ya waislam katika zama za mwisho. Hali ambayo alisema kuwa suluhisho lake lilokuwa ni ujio wa Masihi Aliyeahidiwa.Alibainisha pia ya kwamba kazi ya Masihi na Mahdi haikuwa kuleta dini wala sheria mpya. Bali ilikuwa ni kusuluhisha uma wa waislam, kwa kuwarudisha katika mafundisho halisi yaliyoletwa na Mtume Mtukufu, Muhammad saw. Alihitimisha hotuba yake kwa kuelezea baraka za ukhalifa zilizotokana na ujio wa Masihi na Mahdi, Mwasisi wa jamaat Ahmadiyya iliyo chini ya ukhalifa wa kimbingu hadi sasa.

Mada ya tatu ilikuwa ni juu ya historia ya jamaat Ahmadiyya katika kanda ya ziwa. Hii ilitolewa na Rais wa Jamaat Mkoa wa Shinyanga, Bw. Yusuf Mgeleka. Alianza kwa kuelezea ujio wa mbashiri wa kwanza wa Ahmadiyya katika kanda ya ziwa. ***Sheikh Ahmad Munir aliyefika Kahama mwaka 1957*** kwa ajili ya tabligh, ambapo hakupata mwitikio wowote. Aliongeza kuwa mwaka 1973, aliyekuwa Amir na Mbashiri mkuu wa Tanzania wakati huo, Sheikh Jamil R. Rafiq, alifika Mwanza na Simiyu na kufanya mahubiri, ambapo mzee Thani alijiunga kupitia mahubiri hayo. Aliongeza pia kuwa mahubiri mengine yaliwahi kufikishwa katika kanda hiyo mnamo mwaka 1977 kupitia Sheikh Yusuf Kambaulaya Sahib.



Bw Mgeleka aliendelea kwa kubainisha kuwa mnamo mwaka 2008, Mwl Twaliati Zubeir alifanikiwa kuwa mbashiri wa kwanza wa kiahmadiyya kufungua matawi katika mkoa wa Shinyanga. Alifungua matawi mawili katika vijiji vya Negezi na Bugimbagu katika wilaya ya Shinyanga. Alisema kuwa mapinduzi makubwa ya kimahubiri katika mkoa wa Shinyanga yaliibuka mnamo mwaka 2012. Hayo yalifuatia ziara ya Amir Sahib mkoani humo, ambapo alizuru matawi hayo baada ya kuhudhuria mkutano wa amani, ulioandaliwa na jamaat huko Mwanza.

Baada ya kuvutiwa na mwitiko wa watu juu ya mahubiri ya jamaat, Amir Sahib aliamua kutuma idadi kubwa ya walimu katika mkoa wa Shinyanga. Hali hii ikaleta mabadiliko chanya ya kijamaat mkoani Shinyanga. Alitanabahisha kuwa hadi sasa jamaat Ahmadiyya imeshajenga misikiti 29 na nyumba 9 za walimu katika mkoa wa Shinyanga pekee. Pia jamaat imeshachimba visima vya maji vipatavyo 50 katika mikoa ya kanda ya ziwa.

Bw. Mgeleka alihitimisha hotuba yake kwa kuwaomba wanajumuiya wamwombee sana Khalifa wa zama, Amir wa nchi, masheikh na walimu wote wa jamaat, waliofanya juhudi kubwa kuhakikisha ujumbe wa Islam Ahmadiyyat unasmabaa katika kanda ya ziwa ambako idadi kubwa ya wakazi wake walikuwa ni watu wasio na dini.

Baada ya mada hiyo, mgeni mwalikwa, Bw Hassan Harun, aliyemwakilisha Mwenyekiti wa CCM wilaya ya kahama alipewa nafasi ya kutoa salamu. Yeye aliipongeza jamaat na kuishukuru kwa jitihaa zake za kuunganisha jamii na kuhubiri amani.

Ugawaji wa zawadi

Baadaye, Sheikh wa mkoa wa Shinyanga, Maulana Ihtisham Latif alisimama na kutoa taarifa fupi ya maendeleo ya jamaat katika kanda ya ziwa. Alibainisha kuwa kwa mwaka huu hadi wakati anatoa taarifa hii tayari, visima 10 vilishakamilika na vingine 13 vilikuwa katika mchakato wa uchimbwaji. Alisema pia kuwa hadi sasa, jamaat Ahmadiyyat imeshajenga misikiti 50 katika kanda ya ziwa.



Kisha Sheikh Ihtisham akaendesha zoezi la ugawaji zawadi kwa wanajumuiya waliofanya vizuri katika kadhia mbali mbali. Miongoni mwa zawadi hizo zilikuwamo pia zawadi za washindi waliopatikana katika mashindano ya kimwili na kielimu yaliyofanyika katika ijtimaa ya kanda ya Khudamul Ahmadiyya, iliyofanyika siku ya tarehe 4, Julai.

Kadhalika zilitolewa zawadi za mahubiri kwa wahubiri wa mkoa wa Shinyanga. Zone ya Tinde iliibuka kidedea kwa kutwaa nafasi ya kwanza katika ukusanyaji wa baiat. Mwl Ramadhani Mrisho wa zone ya Butibu akiibuka mshindi kwa kukusanya baiatbnyingi kulikonwalimu wote wa mkoa huo. Zawadibya muuzaji bora wa vitabu vilikwenda kwa Mwl Salehe Malifedha. Zawadi zote zilikabidhiwa na Amir Sahib kwa washindi.



Aidha jamaat za kanda ya ziwa zilimkabidhi Amir Sahib zawadi maalum ya kumpongeza kwa kufanikisha ujenzi wa misikiti 50 katika kanda hiyo. Mkuu wa wilaya ya Kahama, Mh. Mboni Mohammed Mpita, aliyemwakilisha mkuu wa mkoa mkutanoni hapo naye alikabidhiwa zawadi maalum.

Ukurasa 7

Yesu aliongozwa na nani Nyikani?

Kutoka Uk 1..

haya mawe yawe mikate.

Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.

Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia, ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana imeandikwa, Atakuagizia malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua; Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.

Yesu akamwambia, Tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako.

Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake». (Mathayo 11-4:1)

Mwenyezi Mungu anazo njia kadhaa anazotumia kuwasiliana na waja wake watakatifu ili kuwajulisha mambo mbalimbali yanayo husu ulimwengu huu wa kidunia na ule ulimwengu wa kiroho. Aidha mambo hayo yanaweza kuwa ni yaliyopita zamani au yaliyopo sasa na au yatakayo kuwepo baadae.

Miongoni mwa njia hizo, aya za Kurani Tukufu zinabainisha kwa kusema:

وَمَا كَانَ لِبَشَرٍ أَن يُكَلِّمَهُ اللَّهُ إِلَّا وَحْيًا أَوْ مِن وَرَاءِ حِجَابٍ أَوْ يُرْسِلَ رَسُولًا فَيُوحِيَ بِإِذْنِهِ مَا يَشَاءُ ۚ إِنَّهُ عَلِيٌّ حَكِيمٌ

Na haikuwa kwa mwanadamu kwamba Mwenyezi Mungu amsemeze ila kwa Wahyi (Ufunuo), au kwa nyuma ya pazia, au kumtuma Mjumbe. Naye humfunulia ayatakayo kwa idhini yake. Hakika Yeye ni Mtukufu, Mwenye hekima. (42:52)

Na tena

وَمَا جَعَلْنَا الرُّؤْيَا الَّتِي أَرَيْنَاكَ إِلَّا فِتْنَةً لِّلنَّاسِ

....Na hatukuifanya ndoto tulio kuonyesha ila ni kuwajaribu watu.(17:61)

Sawa na uthibitisho huo wa maandiko kuhusu Mungu njia gani anatumia kuongea na waja wake wapendwa, tunapoitalii historia ya mitume na manabii na baadhi ya waja wema (Wake kwa Waume), kuona jinsi walivyoongea na Mungu, tunakuta ni kweli zilitumika njia hizo zilizo bainishwa hapo juu. Na miongoni mwa hao walio ongea na Mungu kwa kutumia njia hizo ni Yesu.

Kwa ushahidi wa Biblia, tunakuta kuna wakati inaonesha Yesu aliweza kuongea na Mumgu kupitia Roho Mtakatifu, aliyejidhihirisha kwa sura ya (NJIWA).

Pengine tunakuta aliongea na Mungu kwa njia ya sauti kama Biblia isemavyo:-

Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye.(Mathayo 17:5)

Na pengine Aliongea na Mungu kupitia njozi kama vile tukio lililonukuliwa mwanzoni tu mwa maelezo yangu na ambayo ndiyo hasa yatakayojadiliwa kwenye mada hii katika vipengele kadhaa kama vile:-

1. Kukubali kubatizwa na Yohana Mbatizaji
2. Roho Mtakatifu kujionesha kwa sura ya Njiwa.
3. Yesu kupelekwa nyikani ili akakutane na Shetani.
4. Yesu Kuongozwa na Shetani akiwa nyikani.
5. Kufunga siku arobaini usiku na mchana.
6. Kushauriwa kufanya mazingaombwe ya kubadili mawe kuwa mikate.
7. Kushauriwa kujirusha kutoka juu ya mnara hadi chini.
8. Kuoneshwa miliki ya Dunia na kuahidiwa kupatiwa kwa sharti la kumsujudia shetani.
9. Matukio yanayoonesha Kutimia kwa ndoto yake.
10. Mti mwema hutambulika kwa matunda yake.

Nimetangulia mapema kusema kwamba; watakatifu hujulishwa mambo mbalimbali ya ulimwengu wa kidunia na kiroho. Hujulishwa mambo yaliyopita zamani yaliyopo wakati wa sasa na hata yale yatakayo kuwepo wakati ujao.

Kwa maana hiyo Yesu kuongozwa na shetani

nyikani, ilikuwa ni moja ya taarifa ya Mungu Akimjulisha kimethali nini kitajiri baadaye juu ya wanafunzi wake. Bila shaka tukichunguza neno kwa neno kisa chote cha Yesu kupelekwa na shetani huku na huko, tutabaini kwamba; kwa hakika hiyo ilikuwa ni njozi na uaguzi wa njozi hiyo in lazima uangukie kwa wanafunzi wake na mafundisho yake kwamba yataharibiwa na wanafunzi wake kwa sababu ndogo ndogo tu za kidunia. Kwamba, watapata majaribu kutoka kwa baadhi ya viongozi wao ambao pengine watakuwa na nguvu na mamlaka ya ufalme wa kidunia. Hivyo kwa njozi hii ya Yesu, ni wazi kuwa ilikusudia kuelezwa kuhusu wanafunzi wake kukubali kushikilia batili maadamu tu batili hiyo itakuwa imeanzishwa na wafalme wenye nguvu za kidunia kama vile akina Constantine n.k.

Kitendo chenyewe cha Yesu kukubali kuacha mji na kwenda maporini kukaa na shetani kwa muda wa mwezi mmoja na masiku kadhaa, ni bishara inayoonesha wazi kwamba wakristo wenyewe watafanya juhudi kubwa ya kumtafuta shetani alikojificha na kuamua kupiga kambi huko nyikani mpaka pale watapobebwa na kuongozwa na shetani huyo, ndipo mioyo yao itaridhika.

Kwa sababu SHETANI hata kama apate nafasi ya kukaa na mtu siku moja tu, lazima mtu huyo ataathiriwa vibaya sana, sembuse siku arobaini.!!

Simulizi ya ndoto hii imesimuliwa kama ndio matukio ya mwanzo kabisa yaliyo jitokeza katika mwanzo wa historia ya Yesu. Hii pengine ilikuwa inakusudia kujulishwa mapema kwamba viashiria vya kuharibika na kupote kwa wanafunzi wake vitaonekana hata kabla hajafa na kuondoka duniani hapa. Na hali hiyo ndiyo iliyoonekana mara nyingi kwa wanafunzi wake. Biblia yenyewe imerekodi manung›uniko ya mara kwa mara ya bwana Yesu juu ya wanafunzi wake. Hali iliyompelekea Yesu awachukulie wanafunzi wake kama watu wasio na imani japo ndogo kama chembe ya haradali.

Aliwahi kuwaambia, Mbona mmekuwa waoga, enyi wa imani haba?

(Mathayo 8:26)

Akawahi kuwaambia «Enyi kizazi kisichoamini, kilichopotoka, nitakaa pamoja nanyi hata lini? Nitachukuliana nanyi hata lini»?

(Mathayo 17:17)

Na pengine akawaambia, Kwa sababu ya upungufu wa imani yenu. Kwa maana, amin, nawaambia, Mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali mtauambia mlima huu, Ondoka hapa uende kule; nao utaondoka; wala halitakuwako neno lisilowezekana kwenu.

(Mathayo 17:20)

Hivyo kwa uchache huu wa imani, ndio tunaona kwamba, kweli wanafunzi wake baada ya kutengana na Yesu kwa kitambo kidogo tu, walifanya chapu kuchakachua amri za Mungu, kutoka Amri kumi mpaka kutumika Amri nne. Na si hivyo tu, bali sheria kwao ikasemwa kuwa ni laana na hivyo kutupiliwa mbali hata lile agano la milele lililofanywa na Mungu kwa Ibrahim, agano la kutahiriwa, kama inavyothibitika katika kitabu cha Matendo 33-15:1.

(1) YESU KUBATIZWA NA YOHANA M-BATIZAJI.

Tunaposoma Mathayo 5:17--19

Tunakuta Yesu anasema hakuja kutangua torati na manabii bali kutimiliza. Yaani kuikubali na kuifuata torati na kuwakubali na kuwaamini manabii wa mbele yake.

Akithibitisha hilo kwa vitendo, alikubali kubatizwa na Yohana Mbatizaji na hivyo kumpendeza Mungu, kiasi cha mbingu kufunguka na Roho Mtakatifu kushuka juu yake na huku sauti ikasikika

katoka mbinguni ikisema; «Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe». Marko 1:11.

(2) KUONEKANA ROHO MTAKATIFU KWA SURA YA NJIWA.

Kuonekana Roho Mtakatifu kwa sura ya NJIWA ni dhahiri shahiri mafundisho ya Yesu hayakutakiwa yawe ya kudumu kwa mwanadamu. Hata yeye mwenyewe anatuthibitishia hakutumwa kwa watu WOTE, ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israel tu. Mathayo 15:24;

Na kwa mfano wa baba mwenye shamba, ilionekana kwamba, Yesu lazima atakataliwa kiasi cha kufanyiwa hila za kuuawa na kutupiliwa mbali nje ya wigo, kitendo ambacho Mungu Angeondoa ufalme wake kwa waisraeli na kuwapa watu wengine. Mathayo 21:33--46;

Na kama anavyofahamika NJIWA kuwa ni kiumbe dhaifu sana mbele ya mwanadamu na mwoga asiyeweza kuhimili vurugu za mwanadam na silaha yake kuu ni kuhama (kukimbia) na ndio maana alipokamatwa tu wanafunzi wake WOTE walitimua mbio. Bali na hata mafundisho ya Yesu kwa wanafunzi wake yanadhihirisha jinsi alivyowafundisha kuishi sawa na tabia ya NJIWA, pale aliposema: «Mkifukuzwa mji huu kimbilieni mwengine» Mathayo 10:23

Na kwa kauli ya Mungu mwenyewe vitu vyote amepewa mwanadamu aviongoze, (avitawale). Mwanzo 2:26--28

Sio mwanadamu aongozwe na AKILI ya NJIWA. Hivi ni mwanadamu gani atakayeambiwa ana akili kama ya kuku akaridhika na kufurahi ?? sembuse NJIWA. !!;

(3) YESU KUPELEKWA NA

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Jalsa Salana Uingereza 2023
<Kilele cha Mafanikio Zaidi>

Kutoka uk. 1

hata tumshukuru Mwenyezi Mungu kiasi gani, haitoshi, kwani Yeye alibariki sana kusanyiko hili, na hili lilihisiwa na wote, kwa Waahmadiyya na wageni wasiokuwa Waahmadiyya vile vile. Sisi ni dhaifu; ni kwa baraka za Mwenyezi Mungu tu kwamba tunaweza kufanya lolote, na Jumuiya hii inamiminiwa baraka za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa namna ambayo inaelezwa vyema kuwa:

'Na mkijaribu kuzihesabu neema za Mwenyezi Mungu hamwezi kuzihesabu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu' (Qur'ani Tukufu 16:19).

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anausamehe udhaifu wetu na anatuwekea neema kwa namna ambazo hatuwezi kamwe kumshukuru Yeye. Pamoja na hayo, Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuamrisha kumshukuru, na tukimshukuru, basi Mwenyezi Mungu Mtukufu ataendelea kutupa zaidi. Kwa hiyo ni wajibu wetu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, na tukifanya hivyo, basi tutaendelea kusonga mbele. Kwa hiyo, linapokuja suala la Jalsa Salana, lazima kwanza kabisa tumshukuru Mungu Mwenyezi. Wafanyakazi na wageni wote wanapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Licha ya ukweli kwamba Covid haijatoweka kabisa, Mungu Mwenyezi amemuweka kila mtu salama. Kuna watu wachache ambao, baada ya mkutano, walipata Covid. Hadhrat Khalifatul Masih (atba) aliwaombea kupona. Khalifa mtukufu (atba) alisema kuwa kati ya kesi chache ambazo amezijua, inawezekana kwamba hawakupata Covid kutoka eneo la Jalsa, badala yake, serikali imetangaza kuwa kumekuwa na ongezeko la maambukizi katika maeneo fulani kwa ujumla.

Shukrani kwa Wafanyakazi Wakati wa Jalsa Salana

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba alitaka pia kuwashukuru wafanyakazi, ambao walifanya kazi kwa mtindo wa ajabu, na kwa nyuso za tabasamu kama alivyoshauri hapo mwanzo. Kwa upande wa wanaume na wanawake, wafanyakazi wote walionyesha ustadi mkubwa katika idara zao. Kwa ujumla katika siku za nyuma, kulikuwa na malalamiko kuhusu idara ya kuhudumia chakula. Hata hivyo, mwaka huu, malalamiko hayo yalikuwa hayapo kabisa. Pia kulikuwa na idara za trafiki, upishi, mtambo wa roti na MTA ambao waliunganisha ulimwengu kwa njia mpya mwaka huu. Khalifa mtukufu (atba) alisema idara zote, zile alizozitaja na ambazo hakuzitaja, zote zilifanya kazi nzuri kabisa, wanaume na wanawake, na alitaka kuwashukuru wote.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba hata wageni wasiokuwa Waahmadiyya walionyesha kushangazwa kwao na namna wafanyakazi walivyotekeleza majukumu yao. Mwenyezi Mungu Mtukufu awajaalie malipo bora.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba kuna nukta moja tu ambayo angependa kuvuta mazingatio ya idara ya Jalsa Salana kwayo; maji huzimwa mara tu taratibu za Jalsa zinapoisha. Walakini, maji yanapaswa kubaki kwa angalau saa 12. Vinginevyo, usimamizi ulishika hadhari zote vizuri.

Hisia na Maoni Yanayotolewa na Wageni Waliohudhuria

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba atawasilisha baadhi ya hisia za wasiokuwa Waahmadiyya, hata wageni wasiokuwa Waislamu waliohudhuria Mkutano huo.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) aliwasilisha maoni ya daktari kutoka Burkina Faso ambaye alihudhuria Mkutano huo kwa mara ya kwanza. Alifurahishwa na ukweli kwamba wahudhuriaji wote walikuwa wameunganishwa, wamekusanyika mahali pamoja kwa kusudi moja karibu na kiongozi mmoja. Watu kutoka kote ulimwenguni na kutoka asili tofauti walikuwa wamekusanyika kwa kusudi moja kwa mkono mmoja ambao haukuwa wa kawaida kuonekana. Kiwango cha hotuba kilikuwa cha juu sana. Pia alisikiliza hotuba za Huzur

Ukurasa wa 11

Kuwapiga Ndege watatu >kwa jiwe Moja<

Na.



Mahmood Hamsin Mubiru
Kiwalani Dar es Salaam

Mtu huweza kupiga Ndege wawili kwa jiwe moja, lakini ibn Kitabu Pazi Sadr Majlis Ansarullah na Daktari, amefanikiwa kuwapiga Ndege watatu kwa jiwe moja. Shumbe Daktari Swaleh.

Kukutana na kiongozi wetu Mpendwa Hazrat Mirza Masroor Ahmad atba ni baraka kubwa na fursa ya kipekee. Bila shaka ulimfikishia salamu zetu. Na bila shaka ulimueleza kuwa tunampenda sana. Na bila shaka ulimuomba aendelee kuiombea nchi yetu. Na ninauhakika ulimwambia atuombee. Tanzania imefanikiwa sana kuwa karibu na Makhalifa wa Masihi Aliyeahidiwa[as]. Khalifatul Masihi wa[II] **Hazrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad[ra]** aliipenda sana nchi hii. Alikuwa anaiombea kila mara, Sheikh Mubarak Ahmad alipomuandikia barua kuhusu nchi hii. Kiongozi wa kiroho aliwahakikishia Waahmadiyya kuwa Tanzania ni nchi yetu. Na Alhamdulillah kukamilisha hili Mwanajamati Muhammad Iqbar Dar akafanikiwa kulipatia Taifa hili jina. Kwa sasa ngazi zote za Taifa hili zimekwisha kiri kuwa aliyebuni jina Tanzania ni Muhammad Iqbar Dar. Raisi mstaafu Dr. Jakaya Mrisho Kikwete alikiri hadharani wakati wa kumbukumbu ya miaka 50 ya uhuru wa Tanzania. Hivi karibuni ofisi ya Bunge Dodoma imetoa kitabu - *Historia ya Bunge la Tanzania 1926 - 2021ISBN 978-9976-88-227-8. Ukurasa wa pili, 'asili ya Jina Tanzania' lililobuniwa na Muhammad Iqbar Dar*. Khalifatul Masihi wa[IV] Hazrat Mirza Tahir Ahmad[rha] alitembelea Tanzania mwaka 1988 akaiombea na kuisifu sana Tanzania, *kwa kusema, kuna kitu katika udongo wa nchi hii, kinachoendelea kuwavutia watu wote waliopata kuishi katika nchi hii. Ndugu hawa waliopata kuishi hapa wanaikumbuka nchi hii kwa mapenzi na kila fursa inapopatika basi wanatoa msaada wa hali na Mali*. Khalifatul Masihi wa[V] Hazrat Mirza Masroor Ahmad atba anaikumbua sana nchi hii hususani lile tukio ambapo watu hawakutoka kwa sababu ya mvua na wakaendelea kusikiliza hotuba ya Huzur. Safari yake ya Mtwara ilileta mapinduzi makubwa katika sehemu hiyo ya Tanzania. Harakati za maendeleo zinakuwa kwa kasi na wengine wanathibitisha kuwa ni safari ya baraka ya Huzur iliyoharakisha maendeleo hayo.

Kuhusu Jalsa Salana ni jambo lenye faida kubwa. Huo sio mkutano wa kawaida umeanzishwa na Nabii wa Allah ili kuongeza Taquwa kwa waaminio. Tanzania haikuwa inafanya vizuri katika upande huu, lakini Alhamdulillah naona mwamko mpya. Na wakati Sadr Majlis Ansarullah alipokutana na Huzur alimwambia awahamasishe Ansarullah ili waweze kuhudhuria Jalsa Salana ya Uingereza ambayo sasa imechukua taswira ya kimataifa. Alhamdulillah tujitahidi kuhudhuria. Historia ya nyuma kuhusu kuhudhuria Jalsa Salana, si mbaya sana Waahmadiyya ambao wamewahi kuhudhuria ni pamoja na Alhaj Salum Kungulilo, Mwl. Omary Mnungu Sahib, Bwana Hassan Taufiq, Bwana Saidi Manoro, Mwl.Abdallah Mbanga, Sheikh Bakr A. Kaluta Sahib, Sheikh Ame Sahib, Mwl. Yahya Kachima, Mwalimu Saidi Mgeleka, Bwana Elias Marwa, Mwalimu Mohammed Mkoka, Mustapha Kapulilo, Sultan Ungando, Issa Mwakitalima, Ali Saidi Mosse, Bwana Abdillah Kombo, Bwana Halili Kungulilo na Bwana Ali Mtotela.

Waahmadiyya tunayofuraha kubwa kukutunuku cheo cha Balozi wa heshima wa nchi yetu. Umefanya kazi kubwa kuitangaza vizuri Tanzania na bila shaka kuipenda nchi ni sehemu ya Imani. Kwa jicho la mbali nawaona wa Ghana wakiwa na vitambaa vyao vimepambwa na na bendera yao yenye nyota nyeusi, Waganda, Wanaijeria nawaona hawawezi kuwa nyuma. Masheikh waliokuja nchini hatuwezi kuwasahau na tunakushukuru kufikisha salamu zote pamoja na ndugu zetu waliopata kuishi nchini. Sheikh Waseem Ahmad Cheema, Sheikh Waseem Ahmad Khan, Sheikh Bashartul Rehman, Sheikh Faiz Ahmad na Bwana Mubarak Lone wote tunawakumbuka kwa mapenzi makubwa na heshima.

Bustani ya Washairi

Kimya

Kimya chetu cha heshima, werevu twapisha Mambo
Kila kitu kukisema, waweza wale wa ng'ambo
Sisi waja we hekima, tulisha toka kitambo
Kimya ni kuzungumza, ogopa alonyamaa.

Huchagua la kusema, Kiswaha au Kimombo
Hupenda sana kuzana, kisha huchagua chambo
Kuamba bila kupima, kwetu waitwa mtambo
Kimya ni kuzungumza, ogopa alonyamaa.

Kadi tamati wa tama, ni tama ya wangu wimbo
Tusamehe ya karima, kila tuendapo kombo
Kwenye njia ya zahama, yenye uvundo na shombo
Kimya ni kuzungumza, ogopa alonyamaa.

Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)
Kiwalani - Migombani.

Mjenzi ndiye mjuzi

Mjenzi ndiye mjuzi, kwakile alokiunda
Aloijenga kurunzi, mbali sana akakwenda
Akiba akamaizi, vifaa akaviunda
Usikatae mitala , mjenzi ndiye mjuzi

Hebu mwangalie kuku, jogoo alokomaa
Matembe wenyeshauku, dhamana humpatia
Waamsha mwanzo siku,namwewe kuwaambia
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Muumbaji anajua, ndiyo mana akasema
Rukisa wewe kuoa, wanawake walowema
Moja Hadi nne oa, kuzidisha sio wema
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Akili yako tumia, mitala ukizuia
Wale wanaobakia, utawa watatulia??
Kama hawatatulia, Nini Sasa chafwatia??
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Akili yako tumia, Nini kitachotokea
Usawa tukitumia, mitala kwa mke pia
Mimba mke kipatia, baba yupi atalea
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Kumbuka nakuambia, Kila mwana anababa
Jini wanazichangia, nusu mama nusu baba
Ugomvi utauzua, kugombania ubaba
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Hayo Kenda nakwambia, kumi hili lisikia
Siku zikishakujia, au mwana ukazaa
Waume tavumilia??au dhambi tawatia
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Mtunzi
Masihi omary stambuli kisagwa

Kioo kinashangaza, uchizi kinatutia
Jicho ukikiangaza, mwenzio tamwangàlia
Jicho kwako atakaza, nachofanya igizia
Sikudanganye kioo, uzuri kweli tabia

Ukicheka atacheka, ukilia nayelia
Kasoro atakuweka, ona hapa unadoa
Uzuri takupachika, wanja umeupatia
Sikudanganye kioo, uzuri kweli tabia.

Kioo onyesha khulka, njema iliyotabia
Kwawatu kutazamika, wapate niigizia
Sisura kudanganyika, nakiburi kikajaa
Sikudanganye kioo, uzuri kweli tabia

Mtunzi wetu

KASIDA

1. يَا عَيْنَ فَيْضِ اللهِ وَ الْعِرْفَانِ
يَسْعٰى اِلَيْكَ الْخَلْقُ كَالظَّمْاٰنِ

Ewe uliye chemchem ya fadhili na maarifa ya Allah! Mahuluku wanakukimbilia kama mwenye kiu.

2. يَا بَحْرَ فَضْلِ الْمُنْعِمِ الْمَنَّانِ
تَهْوِىْ اِلَيْكَ الزُّمَرُ بِالْكِيْزَانِ

Ewe bahari ya fadhili za mwenye kuneemesha na kufanya hisani, makundi ya watu wanaharakia kwako na vikombe vyao.

3. يَا شَمْسَ مُلْكِ الْحُسْنِ وَ الْاِحْسَانِ
نَوَّرْتَ وَجْهَ الْبَرِّ وَ الْعُمْرَانِ

Ewe jua la nchi ya uzuri na ihsani, umeangaza miji na mapori.

4. قَوْمٌ رَأَوْكَ وَ اُمَّةٌ قَدْ اُخْبِرَتْ
مِنْ ذٰلِكَ الْبَدْرِ الَّذِىْ أَصْبَانِىْ

Kaumu moja imekuona na umati mwingine umepewa habari za mwezi mpevu, aliyenifanya kuwa ashiki wake.

5. يَبْكُوْنَ مِنْ ذِكْرِ الْجَمَالِ صَبَابَةً
وَ تَأَلُّمًا مِّنْ لَّوْعَةِ الْهِجْرَانِ

Wanalia kwa kukumbuka uzuri wako kwa huba nyingi, na pia kwa kuumia kwa sababu ya kukaa mbali nawe.

6. وَ أَرَى الْقُلُوْبَ لَدَى الْحَنَاجِرِ كُرْبَةً
وَ أَرَى الْغُرُوْبَ تُسِيْلُهَا الْعَيْنَانِ

Nami naziona nyoyo zimeshafika kwenye halkumu kwa sababu ya kukosa utulivu, na ninaona macho yakitiririsha machozi.

7. يَا مَنْ غَدَا فِىْ نُوْرِهٖ وَ ضِيَائِهٖ
كَالشَّيِّرَيْنِ وَ نَوَّرَ الْمَلَوَانِ

Ewe, ambaye kwa nuru yake na mwanga wake umekuwa kama jua na mwezi; na usiku na mchana umeng'arika.

8. يَا بَدْرَنَا يَا اٰيَةَ الرَّحْمٰنِ
اَهْدَى الْهُدَاةِ وَ اَشْجَعَ الشُّجْعَانِ

Ewe Mwezi wetu Mpevu, Ewe ishara ya Rahmani, Kiongozi wa viongozi wote, na shujaa kuliko mashujaa wote!

Kitabu cha KASIDA
Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Kasida ya kumsifu Mtume Mohammad(saw)

19
تحت السيوف أُريق كالقربان فدم الرجال لصدقهم في حبهم

Tafsiri:
Hivyo damu ya watu ikamwagiwa chini ya panga kama dhabihu kwa sababu ya uhalisi wa upendo wao

Maelezo: Masahaba wa Mtume Mtukufu (saw) walionesha ikhlasi na moyo wa upendo kiasi kwamba hawakusita kujitolea mhanga njiani kwa Allah. Sababu pekee iliyowapelekea kufanya hivi ni mahaba na upendo kwa Mola wao na Mtume wake (saw). Kutokana na upendo huo hawakujali hata maisha yao bali walitoka kifuambele ili kuitetea dini tukufu ya Uislamu.

20
فسترتهم بملاحف الإيمان جاؤوك منهوبين كالعريان

Tafsiri:
Walikujia wakiwa wamenyang'anywa (mali yote) kana kwamba walikuwa rabana nawe ukawafunika kwa mashuka ya imani

Maelezo: Masahaba walipojiunga na dini tukufu ya Uislamu waliachwa na ndugu na jamaa zao. Kwa kweli hali hii ilikuwa ngumu kwao kana kwamba walinyang'anywa mali zao zote. Lakini waliendelea kupata maarifa ya kidini kwa Mtume Mtukufu (saw) walipata nuru ya imani iliyowafunika na kuwatunza. Nuru hii ilisababisha wamkurubie Allah subhanahu wataalaa na wakapewa jina la *Ashabii kan-nujuum*.

21
فجعلتهم كسبيكة العقيان صادفتهم قوماً كروثٍ ذِلةً

Tafsiri:
Uliwakuta watu (wenye hali) duni kama mavi na ukawageuza kuwa kipande cha dhahabu safi

Maelezo: Masahaba wa Mtume (saw) walionesha mabadiliko makubwa sana katika maisha yao. Kabla ya kujiunga na dini tukufu ya Uislamu walikuwa wakifuata mazoea ya kijinga lakini baada ya kupata malezi bora kwa Mtume Mtukufu (saw) thamani yao ikaongezeka. Walikuwa wenye faida kubwa kwa watu wengine na hata sasa watu wanaendelea kuiga mifano yao ili kuleta mageuzi katika maisha yao.

Shahabu Ahmad
Morogoro

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Mfalme na Mkulima

Mfalme alikuwa na shamba la matunda. Alikuwa na aina za miti ya matunda ambayo ilikuwa imepandwa hapo. Akaajiri mkulima aliyefahamu kazi, kuitunza miti hiyo ya matunda. Kila siku, mkulima alikuwa akichuma matunda yaliyoiva na matamu kutoka kwa miti tofauti na kuyakusanya vikapuni.



Kila siku asubuhi wakati wa mikutano ya Kifalme, mkulima akimpa Mfalme matunda.



Siku moja mkulima alichuma Cheri na kumpelekea Mfalme. Mfalme alikuwa na kisirani. Alipochagua Cheri kuonja lilikuwa chachu, hivyo akamtolea mkulima hasira zake. Katika hasira, alimpiga Cheri hiyo huyo Mtumishi wake. Cheri lilimgonga kichwani, lakini Mtumishi akasema ; "Mungu ni mwenye Rehema!"



Mfalme akastaajabu sana kwa maneno hayo ya huyo Mtumishi wake!

Mfalme akamuuliza Mtumishi wake: "Lazima utakuwa umeumia na kukasirika lakini bado unasema, 'Mungu ni mwenye Rehema.' Kwa nini?

Mtumishi akasema, "Mtukufu Mfalme, nilitaka kukuletea Mananasi siku ya leo, lakini nikabadili nia. Iwapo ungenitupia Nanasi, ningeumia sana. Mungu
Alikuwa wa Rehema hata akanifanya nibadili nia."

Jalsa Salana Kanda ya Ziwa yanoga

...Kutoka uk.3



Baada ya kukamilika kwa zoezi la ugawaji zawadi, mkuu wa wilaya ya Kahama alipewa nafasi ya kuzungumza na hadhara. Alianza kwa kutoa shukurani na pongezi kwajamaat, kisha akawakaribisha wageni wote wilayani humo na kuwataka wajihisi wako nyumbani. Alipongeza ushirikiano unaotolewa na jamaat kwa serikali katika kuleta mshikamano na amani katika jamii. Kadhalika aliwataka viongozi wa kidini kuendelea kuwajenga watoto na watu wazima kimaadili na kiimani.



Pia hakuacha kuelezea juhudi zinazofanywa na Rais, Mh. Dk. Samia za kuleta ustawi wa kijamii nchini kwa kujenga Shule na kufuta ada. Kujenga Hospitali na kuboresha miundo mbinu mbali mbali. Alitanabahisha pia kwamba Mheshimiwa Rais huwa ni msikivu na ni mtu anayepokea sana ushauri wa viongozi wa dini. Hivyo alitaka aungwe mkono katika jitihada zake za kuliletea maendeleo taifa letu. Baada ya hotuba yake, mkuu huyo wa wilaya alikabidhiwa nakala ya Kurani Tukufu pamoja na tafsiri katika kwa Amir Sahib.

Nasaha za Amir Sahib

Hatimaye Amir Sahib alisimama kutoa hotuba ya kufunga jalsa salana hiyo ya kanda ya ziwa. Katika hotuba yake, Amir Sahib alianza kwa kuelezea maana ya baiat na majukumu ya mtu anayejiunga na jamaat. Alifafanua falsafa ya baiat (kujiuza) kwa mujibu wa maelezo yabMasihi Aliyeahidiwa as. Akifafanua juu ya umuhimu wa kushikamana na baiat, Amir Sahib alirejea aya za Kurani Tukufu na hadithi kadhaa za Mtume[saw], zilizoeleza juu ya jambo hilo.



Aidhabalisisitiza juu ya umuhimu wa kubadilia kiroho, huku akiwahakikishia watu ya kwamba dhambi zote husamehewa iwapo zitafanyiwa toba ya kweli. Aliendelea na hotuba yake kwa kufafanua malengo ya jamaat, kwamba ni kufundisha dini na kuimarisha amani. Pia aliagiza uwepo wa kozi mbali mbali kwa ajili ya waahmadiyya wapya. Alisema, kutokana na uhaba wa walimu wanjamaat katika kanda ya ziwa, kuna haja kubwa ya kuwakusanya vijana waliojiunga, kuwapa kozi fupi fupi na baadaye kuwatumia kama waalimu (madaiyan) huko vijijini.

Alihimiza pia juu ya kuwaelimisha watoto, ambao alisema kuwa ni waahmadiyya wa kesho ambao jamaat inapaswa kujivunia.Aliweka wazi kwamba katika mkoa wa Shinyanga pekee kuna matawi 89 ya jamaat, lakini kuna misikiti 29 na walimu 17 tu. Hivyo akashauri watoto wahimizwe kujifunza elimu ya dini ili waje kuwa viongozi wa jamaat katika maeneo yao. Aidha alinasihi kuwa kazi ya kufanya mahubiri isihesabiwe kuwa ni ya wabashiri pekee.

Amir Sahib alihitimisha hotuba yake kwa kusisitiza upendo baina ya watu, huku akikariri kauli mbiu ya jamaat, upendo kwa wote bila chuki kwa yeyote. Mwishowe alitoa shukurani kwa uongozi mzima wa jamaat katika kanda ya ziwa kwa ushirikiano wao uliopelekea kufana kwa jalsa hiyo. Kadhalika alizipongeza Tanzim zote ngazi ya taifa kwa ushiriki wake katika Jalsa hiyo. Pongezi za kipekee zilikwenda kwa Tanzim ya Ansarullah, ambayo alisema mwaka huu imejitolea kwa kiwango kikubwa. Alisema Sadr wa tanzim hiyo na wana majlis wake wanne, walijitolea kuambata na Amir Sahib tangu mwanzo wa ziara yake. Aliwaombea kila la heri pamoja na tanzim nyingine zote

Aliwashukuru wenyeji wa mkutano huo kwa mapokezi na huduma zao bora kwa wageni. Aliwataka waahmadiyya wapya kutojali upinzani, kwani hiyo ni sunna ya manabii. Aliwasihi pia wasijibu kejeli za wapinzani kwa matusi. Bali wawe wavumilivu na waonyeshe upendo na heshima. Mwishowe aliwaombea washiriki wote wa mkutano , Allah Awafikishe makwao kwa salama na Amani.

Mkutano ulifungwa majira ya jioni kwa maombi ya kimya, yaliyoongozwa na Amir Sahib.



Mwisho

Karibu Jalsa Salana ya 52.

Septemba 29, 30 - 01 Qctoba 2023

Dar es Salaam, Tanzania

Jifunze Kuchoma Mishikaki ya Kuku

Na **Mtandao**



Mahitaji:-

» Vidari vya kuku 2, bila ngozi wala mifupa (safisha na katakata vipande vidogo dogo)
» Mafuta 1/4 kikombe
» Chumvi na pilipili manga kiasi
» Kitunguu saumu kilichopondwa kijiko 1 1/2 cha chai
» Tangawizi ilosagwa 1/2 kijiko cha chai
» Maji ya limao 1 dogo au 1/2 kubwa
» Majani ya kotmiri yalokatwa katwa kiasi



Namna ya Kutayarisha:

1. Tia kuku wako pamoja na viungo vyote katika bakuli na changanya vizuri kwa mikono viungo vienee.
2. Funika vizuri na wacha viingie viungo kwa muda wa saa moja unaweza pia kuacha usiku kucha katika fridge kwa ladha zaidi
3. Ukitumia vijiti vya mti basi hakikisha unaviloweka katika maji baridi kwa muda wa nusu saa ili visiungue wakati wa kuchoma
4. Tunga mishikaki yako kwa idadi upendayo na kisha choma au oka hadi ipate kuiva vizuri pande zote mbili.
5. Mishikaki tayari kwa kula kwa sauce upendayo, ukitaka viungo zaidi unaweza tia manjano, binzari nyembamba ya unga na giligilani ya unga au uoendavyo. Furahia!

(kwa oveni moto uwe nyuzi joto 200)

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA^{AS}

KUISHI MAISHA YA UNYENYEKEVU NA UMASKINI

Kwa wacha Mungu kulikuwa na sharti hili kwamba waishi Maisha ya Unyenyekevu na Umaskini. Hili ni tawi moja la ucha Mungu ambalo kwalo tunapaswa kukabiliana na hasira isiyojuzu. Kituo cha mwisho na kigumu cha arifu na masiddiki ni kuepukana tu na ghadhabu. Kiburi na majivuno huzalika kutokana na hasira; na vivyo hivyo, wakati mwingine, hasira yenyewe inakuwa matokeo ya Kiburi na majivuno, kwa sababu hasira hutokea wakati Mtu anapojipendelea nafsi yake kuliko mwingine. (Taarifa ya Jalsa Salana, ١٨٩٧, uk. ٤٩)

Kama nyinyi mnataka Mungu Awe radhi mbinguni, basi mnapaswa muwe na umoja kama ndugu wawili wa tumbo moja. Aliyetukuza zaidi miongoni mwenu ni yule anayeyasamehe zaidi makosa ya nduguye, na mwenye bahati mbaya ni yule anayefanya ukaidi na hasamehi, basi huyo hahusiani nami. (Kashtie Nuh (Safina ya Nuhu), Ruhani Khazain, J. ١٩, uk. ١٢ -١٣)

Ziara ya Prof Abdu Salaam yasababisha Jamaat Ahamdiyya kusajiliwa Nchini Benin

Kutoka Uk wa 12..

ni Rais na Mawaziri ambao hawakuwa wanaijua Jumuiya Ahmadiyya.

Mgeni wao huyo, alifikia Ikulu na kupata mapokezi makubwa ya Kiserikali na kuendelea na shughuli yake iliyomleta nchini Benin. Alifika katika mji mkuu wa nchi hiyo uitwao Cotonou ambao umesheheni misikiti mikubwa na mizuri na kwa heshima yake walitayarishwa Masheikh wakuu wa nchi hiyo pamoja na baadhi ya mawaziri kumsindikiza kwa ajili ya kufanya ibada japo yeye aliamua kufanya ibada mahali alipolala.

Ikafika siku ya Ijumaa, ambayo kwake ni wajibu wenye ulazima aende msikitini kupata ibada hiyo.

Akielezea tukio hilo, Amir wa Jamaat ya Benin Mheshimwa Bissiriou Mohamed Loukouman Adio anasema " aliwauliza msikiti wa Ahmadiyya uko wapi? Na naomba nipelekwe kusali huko". Walimuambia hawaijui ila ngoja wafanye utafiti hapa mjini. Wakati akisubiria majibu hayo akasema anazo taarifa za kuwepo kwa Ahmadiyya hapa jijini Cotonou na nitasali Ijumaa huko.



Prof. Abdul Salaam akisali sala ya Ijuma Masjid Tawheed, nchini Benin, Cotonou mwaka 1987.

Serikali, masheikh, pamoja na ulinzi mkubwa wote walikwenda kwenye msikiti huo ambao ulikuwa dhalili, mdogo, watu wachache, siyo maarufu na hauna hadhi ya ugeni huo kusali pale. Aidha ilikuwa ni kazi kubwa kwa usalama wa ugeni huo.

Ambapo ndipo ambapo Prof Abdu Salaam alisali Ijumaa ambayo iliongozwa na Imam Ahmadiyya. Aidha alipata nafasi ya kuwasalimia ndugu zake wa kiroho na kuishukuru sana Serikali kwa kumpa nafasi ya kuonana na ndugu zake hao, ambapo pia alitumia nafasi hiyo kuwatia moyo kuwa wasione wanyonge kwani ni matajiri wa Imani chini ya Masih Aliyeahidiwa na hivi karibuni watapata heshima wanayostahili, alisema Prof Abdul Salaam. Maneno hayo yaliwachoma baadhi ya watu aliombatana nao.

Baada ya Sala hiyo na Prof Abdul Salaam kuondoka nchini Benin, msikiti huo ulipata umaarufu mkubwa na kuvutia waumini wengi kusali pamoja na udogo na udhaifu wake. Masjid Tawheed kama inavyojulikana kwa fitna za masheikh na baadhi ya viongozi wa Serikali ulifungiwa na Serikali kwa sababu kuwa ungeweza kuvutia watu wengi Zaidi na kuwapoteza kiimani. Aidha Jumuiya ilikuwa haijapata usajili wa kudumu nchini Benin.



Prof. Abdul Salaam akiwasalimia ndugu zake wa kiroho baada ya Sala ya Ijumaa Masjid Tawheed, nchini Benin mwaka 1987.

Fitina hii, ambayo kwa kiasi kikubwa ilisaidia kuifanya Serikali ya Benin kufanya uchunguzi kwa nchi Jirani juu ya Ahmadiyya. Baada ya utafiti na uchunguzi wa kina, Serikali ya Benin ilijiridhisha kuwa Ahmadiyya ambayo Prof Abdul Salaam ni muumini wake ni Taasisi kubwa na haina mashaka katika itikadi zake kwa usalama wa nchi nakuamua kuipa usajili wa kudumu jumuiya nchini Benin bila ya kujali kelele za watu wengine. Msikiti huo kwa sasa una sura tofauti na ni miongoni mwa misikiti mikubwa yenye hadhi nchini Benin.

Amir Sahib anasema Ahmadiyya nchini Benin haitamsahu Prof Abdul Salaam. Allah ibariki Jamaat Ahmadiyya Benin, Allah ibariki Jamaat Ahmadiyya Tanzania.

MATUKIO KATIKA PICHA





















Kalamu kutoka Kanda ya Ziwa

...Kutoka tolro lililopita

KUCHANUA KWA CHEMCHEM YA JAMAAT AHMADIYYA MKOANI SHINYANGA - 7



Yousuph Mgeleka (Muijukuu)

Ilikuwa ni asubuhi ya tarehe 24.10.2019 katika uwanja wa ndege wa Mwanza (Mwanza Airport) majira ya saa tano asubuhi, pale ambapo mji wa Mwanza ulijaaliwa kumpokea Amir Jamaat Ahmadiyya nchini Tanzania Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akianza ziara ya siku 4 kuitembelea mikoa kadhaa ya ukanda wetu. Katika uwanja huo, mpendwa wetu Amir Jamaat alipewa hadhi ya kupokelewa kupitia eneo la wageni mashuhuri nchini yaani (VIP Lounge). Amir Jamaat alilakiwa na baadhi ya wanajamaat wa Mwanza akiwa njiani kuanza ziara yake ya siku 4 kuzitembelea Jamaat za mikoa ya Geita, Simiyu na Shinyanga. Katika ziara yake hiyo Mheshimiwa Amir Jamaat alifuatana na ujumbe wake ambao ni mzee Akram Ahmad ambaye ni Mkurugenzi wa IAAAE na aliyewasili nchini akitokea Uingereza, alikuwepo Maulana Sheikh Abid Bhatt ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Jamia Morogoro, alikuwepo Maulana Sheikh Shafii Memon ambae ni Sheikh wa Mkoa wa Arusha na alikuwepo Maulana Sheikh Basharat Ahmad ambae ni msimamizi mkuu wa idara ya Uchapaji nchini. Siku hiyo kulikuwa na mabadiliko ya ratiba ya ndege ambapo ndege iliyombeba Amir Jamaat ilichelewa kuondoka Dar kwa masaa mawili na hivyo tukapatwa na khofu juu ya ratiba itakavyokuwa. Majira ya saa tano na dakika 10 asubuhi, Alhamdulillah mpendwa wetu Amir Jamaat aliwasili na kupokelewa na viongozi wa Mkoa wa Mwanza wakiongozwa na Rais wa Mkoa wa Mwanza, Naib Rais wa Mkoa wa Mwanza, Naib Sadr MKA Kanda, Katibu Mkuu wa Jamaat mkoani Mwanza

AMIR JAMAAT ZIARANI MKOANI GEITA

Mara baada ya kuwasili Amir Jamaat na kusaini kitabu cha wageni Maalum pale uwanja wa ndege, hatimae ziara rasmi ikaanza kwa kuelekea Mkoa wa Geita. Huko kulikuwa na ufunguzi wa msikiti mmoja katika tawi la Nyamwilolelwa, ambapo licha ya sisi kuchelewa lakini wanajamaat na ndugu waalikwa hawakuchoka kutusubiri. Awali tulitegemea kufika mkoani Geita saa saba mchana lakini tukawasili mkoani humo majira ya saa kumi jioni, lakini wanajamaat wenyeji wetu kwa mapenzi yao makubwa kabisa, hawakuchoka kumsubiri kiongozi wao wa kiroho mheshimiwa Amir Jamaat mpaka alipowasili na kuwafikia hapo tawini Nyamwilolelwa. Na kwa shauku na mapenzi makubwa, wanajamaat kadhaa wa Mwanza wapatao watano nao ilibidi wamsindikize Amir jamaat huko mkoani Geita.

Majira ya saa kumi alasiri, viunga vya kijiji cha Nyamwilolewa kikazizima kwa mapambo makubwa na maalum ya wanajamaat kuuzunguuka msikiti mpya wa Jamaat kwa foleni za watu. Wanajamaa waume kwa wake kwa mistari mirefu na mipana wakiuzunguuka msikiti, Lajna wakiwa na shungi zao zilizopendeza, nasrat wakiwa kwenye sare nzuri na mitandio iliyopendeza, huku wakipaza sauti maarufu za ukaribisho kwa mpendwa wao zilizosikika “Ahlan wa sahlan wa marhaba”. Hakika ilikuwa ni mvuto wa kipekee kabisa. Hali hiyo iliwashangaza ndugu wengi wasiokuwa wanajamaat na ikabidi nao waweze kusogea na kujifunza juu ya namna mgeni wa juu kijamaat alivyopokelewa kwa mapenzi na heshima kubwa. Hakika, mapokezi ya Amir Jamaat mkoani Geita yalitia fora kwa umati mkubwa sana kuja kumpokea, Alhamdulillah.

Katika khutba zake Amir Jamaat na kote alipofika, aliwaasa sana wanajamaat kuitumia misikiti yetu kwa ajili ya ibada. Na kwamba kwa kupitia ibada basi mambo yote maovu yataepukika nasi kuwa ni waumini wema na tegemeo kwa taifa letu. Aidha Amir Jamaat pia alibeba ujumbe wa kuwahimiza na kuwasimamia watoto katika kuwakuza kiimani kwa kuhakikisha wanafundishwa masomo ya dini na kujua kusoma Qur’an. Hapa alisisitiza sana na kuweka mkazo maeneo yote aliyotembelea.

AMIR JAMAAT AKIWA MKOANI SIMIYU

Siku ya Ijumaa asubuhi na mapema safari kuelekea mjini Bariadi mkoani Simiyu ilianza. Msafara wa gari mbili ulimuongoza Amir Jamaat na kufikia saa nne na nusu asubuhi tayari mpendwa Amir Jamaat pamoja na wajumbe wake waliwasili mjini Bariadi na kupokelewa na Rais wa Mkoa huo ndg Hamza Mkoka sanjari na Mwl wa Mkoa wa Simiyu Abdulatif Yusuf Ngalombe na baadhi ya wanajamaat wa mjini Bariadi. Baada ya kuwasili na kupata mapumziko mafupi, hatimae msafara wa Amir Jamaat kuelekea kwenye ufunguzi wa msikiti mpya tawini Ntobo, ilianza. Ambapo mheshimiwa Amir Jamaat aliwasili hapo majira ya saa saba kamili, na kupokelewa na umati wa wanajamaat wengi nae aliwasalimu mmoja baada ya mwingine, na kisha kuufungua msikiti huo na kisha kufanya maombi. Mara tu baada ya maombi, mheshimiwa Amir Jamaat aliongoza swalatul Jumaa katika msikiti huo mpya ambapo msikiti uliweza kujaa wanajamaat wengi wa tawini hapo. Katika Khutba yake ya Ijumaa, mheshimiwa Amir Jamaat aliwaasa wanajamaat wote kuwa “leo hii nyumba ya Allah imefunguliwa, lengo la nyumba hii ni kutekeleza ibada na kumkumbuka Allah. Nyumba hii katu haitumiki kwa masuala ya siasa za aina yeyote ile, bali ni kwa ajili ya Allah tu”. Alieleza Amir Jamaat.

Aidha mara tu baada ya Swalatul Jumaa kukamilika, mheshimiwa Amir Jamaat pamoja na Mheshimiwa mzee Akram Ahmad sahib kwa pamoja walifanya uzinduzi wa kisima cha maji safi hapohapo tawini Ntobo, kisima hicho kilijengwa kwa usimamizi wa idara ya IAAAE mpaka kukamilika. Alhamdulillah kisima hicho kitasaidia huduma hapo msikitini na pia kitawatua ndoo akina mama wa tawi la Ntobo mkoani Simiyu. Hapo Amir Jamaat alishuhudia maji safi yakitoka, maji salama kabisa kwa matumizi ya mwanaadam. Kisha Amir Jamaat na Mkurugenzi wa IAAAE kwa pamoja waligawa tamtam kwa watoto waliokuwepo hapo yaani (Atfal na Nasrat), watoto hao walifurahi sana kwa uwepo wa kiongozi wao wa kitaifa. Alhamdulillah.

Baada ya hapo msafara wa mheshimiwa Amir Jamaat na wajumbe wake ulielekea tawi la Mitobo, ambapo hapo alifaulu pia kupokelewa kwa uwingi wa wanajamaat na kisha akapata nafasi ya kuifungua rasmi nyumba mpya ya mwalimu ijulikanayo kama (mission house). Akiwa ameambatana na Mkurugenzi Mkuu wa IAAAE, mheshimiwa Amir Jamaat alipata kufungua nyumba hiyo kwa kukata utepe na kisha kuongoza kufanya maombi kwa wanajamaat wote tawini hapo. Pamoja na mambo mengine, mheshimiwa Amir Jamaat pamoja na Mkurugenzi wa IAAAE mzee Akram sahib, baada ya ufunguzi huo wa kisima waligawa peremende kwa watoto (Atfal na Nasrat) waliokuwepo hapo, waliopanga mistari na kugawiwa kwa ustaarabu na utulivu mkubwa. Na hapo ndio ikawa mwisho wa ziara mkoani Simiyu, jioni Mheshimiwa Amir Jamaat alirejea Bariadi mjini kwa mapumziko.

AMIR JAMAAT AKIWA MKOANI SHINYANGA

Ni majira ya saa tano asubuhi, mheshimiwa Amir Jamaat aliwasili mkoani Shinyanga na kupokelewa na Rais wa Mkoa huo pamoja na Mwl wa Mkoa huo, ambapo moja kwa moja mheshimiwa Amir Jamaat alielekea katika tawi la Negezi kwa ajili ya ufunguzi wa nyumba mpya ya mwalimu wa Jamaat ijulikanayo kama (mission house).
Mara tu baada ya kufika, mheshimiwa Amir Jamaat pamoja na Mkurugenzi wa IAAAE walilakiwa kwa furaha tele iliyoambatana na viitikio vya Ahlan wa sahlan wa marhaba. Ndugu wanajamaat walipanga safu ndefu ili kumlaki mgeni wao mpendwa, ambapo mheshiiwa Amir Jamaat aliwasalimu ndugu wote kwa kushikana nao mikono na kisha kuelekea kuifungua nyumba mpya ya mwalimu. Baada ya ufunguzi, mheshimiwa Amir Jamaat aliongoza maombi kwa wote na kisha ndugu wote kuelekea msikitini kwa ajili ya swalatul dhuhr.
Mara tu baada ya sala, Mheshimiwa Amir Jamaat aliongea na wanajamaat wote ndani ya msikiti na kuendeleza ujumbe aliokuja nao kwa ukanda wetu. Akiwa katika tawi hilo, mheshimiwa Amir Jamaat aliwahimiza na kuwasisitiza sana wanajamaat kuhakikisha watoto wao anajua kusoma Qur’an na pia wanajua mazingatio yote ya sala. Alifafanua zaidi mheshimiwa Amir Jamaat. Ndugu wenyeji wa tawi hilo walimuandalia pia chakula mgeni wao na kula kwa pamoja.

Baada ya kusikia juu ya ujio wa Amir Jamaat mkoani Shinyanga, wanajamaat wa tawi la Nsalala walimuomba Amir Jamaat afike tawini kwao na awasalimu kwani walieleza kuwa wanajamaat wa hapo walijawa na hamu ya kufikiwa na ugeni wa Amir jamaat. Naam, majira ya alasiri, msafara wa Amir Jamaat ulifika tawini Nsalala na kulakiwa na Rais wa tawi hilo akiwa pamoja na Mwl wa tawini hapo. Mheshimiwa Amir Jamaat aliwasalimu wanajamaat wote kwa kushikana nao mikono na kisha kuelekea msikitini ambapo aliongoza kikao kifupi cha kuwasalimu wanajamaat wa tawini hapo. Mheshimiwa Amir Jamaat aliwakumbusha wanajamaat wa Nsalala kuwa daima wakumbuke kuwa wao ni wanajamaat wa mwanzo kabisa ndani ya mkoa huo, hivyo yawapasa wakumbuke majukumu yao kijamaat na wautendee haki msikiti uliopo tawini hapo kwa kutekeleza ibada, yaani sala tano kwa nyakati. Hapa mheshimiw Amir Jamaat alitumia muda mfupi wa nusu saa tu, kwani alikuwa akisubiriwa matawi mengine mawili kwa ajili ya ufunguzi wa visima.

Majira ya saa kumi na nusu msafara wa Amir Jamaat uliondoka tawini Nsalala na kuelekea katika tawi la Kidanda ambapo huko kulikuwa na uzinduzi wa kisima cha maji safi kwa matumizi ya mwanaadam. Majira ya saa kumi na moja na nusu msafara ulifika tawini Kidanda na kupokelewa na Rais wa hapo akiwa sambamba na mwal husika wa tawi hilo, na alilakiwa na wanajamaat wa hapo. Mara baada ya kusalimiana, mheshimiwa Amir Jamaat aliongozana na Mkurugenzi wa IAAAE duniani mzee Akram sahib kwenda kufungua kisima kilichochimbwa na kujengwa na Jamaat, hapo walikata utepe na kufuatiwa na maombi yaliyoongozwa na Amir Jamaat. Na mara baada ya hapo, kama kawaida mheshimiwa Amir Jamaat pamoja na Mkurugenzi wa IAAAE walijaza ndoo ya maji safi na salama na kisha kumkabidhi mmoja wa Lajna wa hapo ikiwa ni ishara ya kuwatua ndoo mama zetu kwa tatizo sugu la maji vijijini katika ukanda wetu. Baadae Amir Jamaat aliongea na wanajamaat wa hapo na kuendeleza msisitizo wa ujumbe aliokuja nao awamu hii, kisha mpendwa Amir Jamaat aliwaaga wanajamaat wote wa hapo na kuondoka.
Kwa kuwa jua tayari lilikuwa karibu kuzama, mheshimiwa Amir Jamaat ilibidi aahirishe ufunguzi wa kisima tawini Sungamile (sawa na muda kuisha) na hatimae alielekea moja kwa moja mjini Kahama tawini na kusali sala ya Maghrib hapo, na baadae kupumzika kwa kujiandaa na ziara siku inayofuata.

Mapema siku ya Jumapili asubuhi, mheshimiwa Amir Jamaat alielekea wilayani Ushetu kwenda kufungua visima viwili na msikiti mmoja. Alianzia katika tawi la Mulungu ambapo hapo alifungua kisima, akaongoza maombi na kisha aligawa tamtam kwa watoto yaani (Atfal na Nasrat). Na alimalizia kwa kufanya kikao kifupi na wanajamaat wa hapo kabla hajaendelea na ziara maeneo mengine.

Saa sita na dakika 45 mchana, mheshimiwa Amir Jamaat alifika katika tawi la Mwabayanda, ni umbali wa masaa mawili kutoka Kahama mjini. Huko Amir Jamaat aliufungua msikiti mpya tawini hapo, akaongoza maombi na kisha swalat dhuhr ilisaliwa ndani ya msikiti huo. Mara baada ya sala kulikuwa na hafla iliyoandaliwa na wenyeji wanajamaat wa tawi hilo na walialikwa viongozi wa serikali pia. Ambapo Amir Jamaat aliongoza hafla hiyo na aliendeleza ujumbe wake kuwa “misikiti imejengwa kwa ajili ya ibada, hivyo wanajamaat wa hapo wajitahidi kuuthamini msikiti huo na wautendee haki kwa kumiminika kusali sala tano kila siku”. Aliendelea kufafanua Amir Jamaat.

Kisha ikafuata zamu ya uzinduzi wa kisima ambapo Mheshimiwa Amir Jamaat alikata utepe na kisha kuongoza maombi na kujaza ndoo maji ikiwa ni ishara ya kutatua tatizo sugu la maji vijijini. Wakati wa uzinduzi huo wa kisima, Mwenyekiti wa kijiji hicho, Afisa mtendaji wa kijiji walitoa maneno ya shukrani kwa Jamaat Ahmadiyya kwa kuwakumbuka na kuwatatulia kadhia kubwa ya tatizo la maji kijijini hapo. Walishukuru sana.
Majira ya saa kumi jioni Mheshimiwa Amir Jamaat alianza safari ya kurejea mjini Kahama kwa mapumziko jioni hiyo.

MIUJIZA NA MSAADA WA ALLAH KATIKA ZIARA YA AMIR JAMAAT.

Wiki moja kabla ya ziara, ukanda mzima wa Ziwa ulianza kugubikwa na neema ya mvua, ambapo mikoa yote kusudiwa kwenye ziara ya Amir Jamaat mvua kubwa zilianza kunyesha
Nakumbuka, siku mbili kabla mheshimiwa Amir Jamaat kuja ukanda wetu, nilikuwa tawini Mwabayanda wilayani Ushetu mkoani Shinyanga. Huko nilikuwa pamoja na Mwl Abdulghani Msimbe pamoja na Mwl Abdallah Difika, kuanzia saa tisa alasiri mvua kubwa sana ilinyesha tena yenye upepo mkali na ngurumo nyingi. Hapo tulikuwa na kazi kadhaa za kumalizia kabla ya ujio wa Amir Jamaat, sisi tukajiuliza hivi na mvua hizi itakuwaje siku Amir sahib akija na wanajamaat wamejaa kwa wingi itakuwaje? Maana msikiti ni mdogo haututoshi pamoja na waalikwa. Nakumbuka siku hiyo nilibeba maturubai matatu ili kuyaacha pale tawini Mwabayanda kwa dharura, ila baada ya mvua ile ilibidi tuongeze maturubai mengine manne ili siku hiyo mvua ikinyesha basi tusitirike. Na siku hiyohiyo nikiwa tawini Mwabayanda Amir Jamaat alinipigia simu kujua hali ya maandalizi ilivyo huko, wakati tunaongea alibaini kuwa mvua inanyesha. Amir Jamaat akaniuliza, je mvua inanyesha hapo hivi sasa? Nikamjibu kuwa ndio mvua inanyesha tena kubwa sana, akasema loh itakuwaje sasa na hizo njia zitapitika kweli kuwafikia wanajamaat? Nikamjibu tumuombe sana Allah atatusaidia tu mheshimiwa Amir sahib, ziara itakamilika tu Insha Allah.

Siku ya Jumatano, yaani siku moja kabla Mheshimiwa Amir Jamaat kuja, nikiwa Mwanza mjini nilishuhudia mvua kubwa sana ikinyesha na sisi sote kupatwa na khofu kuwa itakuwaje juu ya ziara ya Amir Jamaat na mvua hizi, tukajiuliza hivi hatutaharibikiwa kweli? Tulijiuliza tukiwa Markaz Mwanza mjini sambamba na bwn Abdallah Mgunya na ndugu Yunus Bakari, tukasema aah ngoja tumuachie Allah mwenyewe.
Kesho yake yaani siku ya Alhamisi tukiwa njiani kuelekea mkoani Geita, nilipokea simu kutoka kwa Mwl Ramadhan Mahmood. Ilikuwa ni majira ya saa nane hivi akinieleza kuwa naomba mngejitahidi kuwahi kufika kwani muda wowote mvua itanyesha hapa maana kuna wingu zito limetanda. Mimi nikamwambia kuwa sawa tunajitahidi kuwahi kufika huko, muda huo maalim Mahmood alikata tamaa ya kwamba sasa itakuwaje na mvua hii na mapokezi ya Amir Jamaat, mbona hii itakuwa ni kadhia. Nilimwambia kwa ufupi sana kuwa Maalim tumuachie Allah.
Maeneo yote tukapita mvua imenyesha, mpaka tawi jirani na tuendapo mvua kubwa sana ilinyesha. Maajabu ni kwamba pale tawini Nyamwilolelwa mvua haikunyesha kabisa na palikuwa ni pakavu kabisa, ilhali vijiji vyote vinavyozunguuka kijiji cha Nyamwilolelwa siku hiyo mvua ilinyesha. Hapo tawini Nyamwilolelwa Amir Jamaat alifika salama na ugeni wake, shughuli iliisha salama na kuondoka salama pasipo mvua kunyesha kabisa. Kudra za Allah hizi.

Mkoani Simiyu napo mvua zanyesha kila siku, lakini kila tawi tunapokwenda ni ama mvua imenyesha au itanyesha. Lakini hapakuwepo na mvua kunyesha wakati Maulana Amir sahib yupo, hapakuwa na mvua kunyesha mpaka amemaliza ziara mkoani Simiyu. Yaani kila tunapokamilisha ziara, basi nyuma yake ndio mvua inaendelea kunyesha. Allah sub’hanahu wa ta’ala alikuwa akituteremshia neema ya nusra ili kazi zake zikamilike kisha neema ya mvua iendelee kumiminika. Alhamdulillah.

Hali kadhalika mkoani Shinyanga, licha ya mvua nyingi na kubwa kunyesha lakini kila Amir Jamaat alipokanyaga ni ama mvua ilinyesha au mvua tanyesha baada ya kumaliza ziara tawini hapo.
Maajabu ni kwamba, mara tu baada ya kumaliza ziara na kurejea jijini Mwanza, mvua ilianza kunyesha siku ya Jumatatu jioni yote mpaka saa nne usiku mvua ilinyesha tu, na asubuhi ya Jumanne siku ambayo Amir Jamaat alikuwa anaondoka mvua kubwa sana ilinyesha. Mimi pamoja na Masheikh walioambatana na Amir Jamaat tukazidi kuulizana, huu ni muujiza mkubwa sana. Kabla ya ziara (kwa sisi wenyeji) ilikuwa kila mtu akihofia je huko vijijini kutaendeka kweli na Amir Jamaat kutimiza ziara zake kama ilivyokusudiwa? Lakini ni msaada mkubwa sana wa Allah tulioupata katika ziara ya kiongozi wetu mpendwa. Jambo hili linatukumbusha sana sisi waaminio kumtegemea Allah nyakati zote, kwenye mambo yasiyowezekana basi kwa Allah yanawezekana tumtegemeapo na tumuombapo. Hakika ziara hii ya Amir Jamaat imetupatia fundisho kubwa na lisilosahaulika, maana khofu zote Allah aliziondoa na akatusafishia njia ili tu kuweza kumfikisha kwa usalama alipopakusudia kufika kiongozi wetu Amir Jamaat.

Siku ya kuondoka kurejea markaz jijini Dar, mheshimiwa Amir Jamaat pamoja na wajumbe alioambatana nao walijaaliwa kupewa hadhi ya kutumia eneo la VIP ya uwanja wa ndege wa Mwanza wakati akiondoka. Siku hiyo tena Mheshimiwa Amir Jamaat alichelewa kuondoka Mwanza kwa masaa mawili zaidi, hii ilitokana na hali ya hewa kutokuwa nzuri kufuatia mvua kubwa zilizoendelea kunyesha na mawingu mazito kutanda angani na ndege kushindwa kutua au kuruka kwa wakati. Hivyo mheshimiwa Amir Jamaat alibaki katika ukumbi wa VIP airport jijini Mwanza kwa masaa mawili hapo, huku Allah akijaali huduma zote akihudumiwa katika Lounge hiyo, huu ni msaada mkubwa wa Allah kwa namna anavyoinyenyua na kuipa hadhi Jamaat yake. Ilipofika saa saba mchana ndipo Amir Jamaat waliondoka na Alhamdulillah walifika salama kabisa jijini Dar bila bughudha zozote. Hakika maneno mazuri ya shukrani kwa Allah Mtukufu ni Alhamdulillah Rabbil Alameen.

Mwandishi wa makala haya alishiriki kwa ukamilifu ziara nzima ya mpendwa wetu Mheshimiwa Amir sahib, kuanzia mwanzo mpaka mwisho.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Jalsa Salana Uingereza 2023: Kilele cha Mafanikio Zaidi

Kutoka uk. 5

Aqdas (atba), ambazo zilifungua macho yake kuona umuhimu wa ulimwengu kutambua ujumbe wa Mungu. Pia alitambua uhusiano wa ajabu walio nao Waahmadiyya na Mungu na kiongozi wao. Alieleza nia yake, ikiwezekana, kuhudhuria Jalsa Salana kila mwaka.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kuwa Dk. Brad Shaw, profesa maarufu wa Sheria kutoka Marekani, pia alihudhuria Mkutano huo. Alisema kwamba alifurahi sana kuona mkusanyiko huo mkubwa. Anasema kuwa pia ameendesha makongamano mbalimbali ambapo usajili unahitajika, hata hivyo, namna ya kupangwa kwa usajili katika Mkutano huo kwa dakika chache tu ilikuwa ya kushangaza. Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alipongeza kazi iliyofanywa na idara ya usajili. Daktari huyo wa Marekani alipongeza jitihada za wafanyakazi wote aliokutana nao.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba Meya kutoka Belize pia alihudhuria Mkutano huo. Alisema katika maisha yake hajawahi kuona watu wenye amani na upendo kama hao. Alieleza kushangazwa kwake kwamba watu wanahusisha ugaidi na Uislamu. Alisema kwamba hali ya kiroho na upendo wa pande zote aliona ni jambo la kupongezwa sana. Alitiwa moyo sana hivi kwamba alionyesha tamaa yake ya kuhudhuria wakati ujao, si kama Meya, bali kama mfanyakazi. Anasema kwamba hajawahi kuona kusanyiko la ajabu kama hilo. Anasema kwamba mustakabali wa dunia ni Ahmadiyyat.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kuwa Michael Wilson, mgeni kutoka Ghana, pia alihudhuria. Yeye ni mwanateknolojia mkuu chini ya Idara ya Sayansi ya Mazingira na Teknolojia. Pia anahudhuria mikutano mbalimbali duniani. Hata kabla ya Jalsa kuanza, alishangazwa na kazi iliyokuwa ikifanywa na kueleza kuwa haiwezi kufanyika bila neema ya Mungu. Baada ya kuiona Jalsa halisi, alishangazwa na kujitolea kwa wafanyakazi wa Jalsa na akaeleza kwamba lazima iwe ni neema ya Mungu. Alishangazwa na ukweli kwamba watu wanaofanya kazi katika nyanja fulani za kitaaluma walikuwa wakifanya kazi tofauti kwenye Jalsa. Pia alishangazwa na tukio la Bai'at ya Kimataifa na akaeleza nia yake ya kuhudhuria katika siku zijazo. Alisema Jumuiya ya Ghana inapaswa kufanya zaidi kuwatambulisha watu wa Ghana kwenye Jumuiya ya Ahmadiyya.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kuwa Waziri wa Habari kutoka Gambia pia alihudhuria, ambaye alishangazwa na kazi ya kujitolea inayofanywa na wale waliotoa huduma. Hakukuwa na tukio hata moja la ugomvi wowote katika mkusanyiko mkubwa kama huo. Upendo wa wanajumuia kwa kiongozi wao hauna mfano. Hakuna taswira bora ya kiutendaji ya udugu kuliko mfano unaoonyeshwa na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba mwanahistoria na mtunza kumbukumbu kutoka Uhispania pia alihudhuria Jalsa Salana ambaye hajawahi kuona watu wengi wa asili tofauti wamekusanyika mahali pamoja. Alieleza kwamba Jumuiya ya Ahmadiyya imeonyesha mfano bora wa juhudi na ustahimilivu, ambao atautekeleza katika maisha yake mwenyewe.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba mwandishi kutoka Italia aliyehudhuria alisema kwamba walikuwa wamesikia kuhusu Jalsa Salana, lakini kuhudhuria ilikuwa tukio tofauti kabisa. Walivutiwa sana na kujitolea, upambaji na usafi, jambo ambalo si kitu rahisi katika mkusanyiko huo mkubwa. Pia walivutiwa sana na Swala ilivyoswaliwa. Ingawa hawakuwa Waislamu, walisema kwamba namna Waahmadiyya wanavyoswali ni jukumu kuu la kila mtu.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba mgeni kutoka Columbia alivutiwa na hali ya amani na upendo na hotuba za Hadhrat Khalifatul Masih (atba). Alisema kwa kuona kusanyiko hili, tunapaswa kujua kwamba licha ya nyakati ngumu, Mungu yuko pamoja nasi. Alistaajabishwa na mpangilio na wafanyakazi, ambao aliwaona kila mahali wakifanya kazi kwa nyuso zenye tabasamu. Kujitolea huku ni mfano kwa ulimwengu na kwa wale wanaomtafuta Mungu.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba Padre Mkristo na mwanatheolojia kutoka Chile pia alihudhuria. Alivutiwa na umoja na udugu wa Jumuiya. Anasema kwamba amehudhuria mikutano mingi ya Kikristo ulimwenguni pote, lakini hajawahi kuona tengenezo kubwa kama hilo likiratibiwa na wanaojitolea popote pengine. Kwa maoni yake, mafanikio ya Mkutano huu yanatokana na umoja wa Jumuiya kuhusu kiongozi wao. Aliitaja Jumuiya kuwa ni chombo; Khalifa ni kichwa na ubongo, na Wanajumuiya ni viungo vinavyofanya kazi kulingana na ishara zinazotumwa kutoka kwenye ubongo.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema Makamu Mkuu wa wenyeji wa asili kutoka Canada pia alihudhuria, na alifurahishwa sana na sherehe ya Bai'at ya Kimataifa. Yeye, pia, akawa na hisia, kama kila mtu. Anasema kwamba hakuwahi kupata hali ya kiroho kama hiyo aliyoipata wakati wa tukio la Bai'at.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba watu wanaotazama duniani kote pia walionyesha hisia zao. Mgeni Mkristo nchini Kongo-Brazzaville alijiunga na Jumuiya kwa kutazama kikao cha kuhitimisha Jalsa. Baadaye, alisema kwamba kama mambo aliyosema Khalifa mtukufu (atba) yatatekelezwa, basi hakuna hata mtu mmoja duniani ambaye angelala njaa. Alisema kwamba moyo wake ulikuwa umetulia kwa sababu ya namna ambayo 'Khalifa wetu' aliwasilisha Uislamu. Alieleza kwamba alisema 'Khalifa wetu' kwa sababu 'kuanzia leo niko pamoja nanyi, na sasa yeye ni Khalifa wangu pia.'

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba baadhi ya watu wanaotazama Jalsa duniani kote hata waliukubali Uislamu Ahmadiyya kama matokeo yake, kwa mfano, kutoka Guinea-Bissau na Tanzania.

(Hii ni mifano michache tu ya hisia mbalimbali za wageni zilizowasilishwa na Khalifa mtukufu (atba).

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba alipokea hisia na maelezo mengi kutoka kwa wageni, ambayo yote hayawezi kusomwa.

Madhumuni ya Kweli ya Mkusanyiko wa Kila Mwaka na Uhabarishaji

Khalifa mtukufu (atba) aliomba kwamba matokeo ya Jalsa hii yawe kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu awawezeshe Waahmadiyya waendelee kushikamana na Mwenyezi Mungu katika maisha yao yote, waongezeke katika imani na yakini, na wawe ni wale wanaotimiza lengo la ujio wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Na athari kwa wasio-Ahmadiyyah isiwe ya muda, badala yake, iwe yenye kuyafumbua macho daima. Na watambue mafundisho ya Uislamu Ahmadiyya kuwa ndiyo njia ya kweli ya wokovu kwao na kwa ulimwengu wote.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba Jalsa ilisikika kupitia aina mbalimbali za vyombo vya habari. Idhaa 24 barani Afrika zilitoa hotuba zote za Hadhrat Khalifatul Masih (atba), na kuwafikia zaidi ya watu milioni 40. Wakurugenzi 23 wa vyombo vya habari na waandishi wa habari walitembelea Kituo cha Vyombo vya Habari huko Jalsa, ambao walitayarisha ripoti za habari kila siku, matokeo yake ripoti 72 zilitayarishwa, na kuwafikia takriban watu milioni 50. Tovuti 41 zilichapisha ripoti, na inakadiriwa kuwa wasomaji ni milioni 19. Magazeti 15 yaliandika juu ya Jalsa, yenye wasomaji wanaokadiriwa kufikia milioni 15. Ripoti 14 za habari za TV zilionyeshwa, na inakadiriwa kuwa watazamaji ni milioni 20. Ripoti 37 zilirushwa kwenye redio, huku takriban watu milioni 8 wakisikiliza. Idhaa mbalimbali, kama vile BBC na nyinginezo kutoka duniani kote ziliangazia Jalsa, na hivyo kutambulisha Uislamu Ahmadiyya.

Khalifa mtukufu (atba) alituombea kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu atuwezeshe kubaki wanyenyekevu na kuendelea kujirekebisha, na tubaki daima kushikamana na Jumuiya, huku tukitimiza madhumuni ya ujio wa Masihi Aliyeahidiwa (as).

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

HABARI UK> 4

Yesu aliongozwa na nani Nyikani?



HABARI UK> 10

Kalamu kutoka Kanda ya Ziwa

Kupiga Ndege watatu kwa jiwe Moja

HABARI UK> 5

Ziara ya Prof Abdu Salaam yasababisha Jamaat Ahamdiyya kusajiliwa Nchini Benin

Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Islamabad, UK

Ilikuwa mnamo mwaka 1987, ambapo Serikali ya Benin ilimualika Prof Abdu Salaam ambaye ni mshindi wa nishani Nobel katika Sayansi ya Fizikia, kufungua Chuo kikuu cha Hisabati katika nchi hiyo.

Katika Serikali hiyo ambao walishiriki kutoa mualiko huo

HABARI UK> 8

Prof. Abdul Salaam akisali sala ya Ijuma Masjid Tawheed, nchini Benin, Cotonou mwaka 1987.



Tohfatun-Nadwah
[Swahili Translation]

"Vipi mdai wa uwongo wa Utume anaweza kufananishwa na mimi? Nimeungwa mkono na miujiza mingi. Mafanikio yangu yanatoka kwa Mungu na ni utimilifu wa ahadi Zake. Haiko ndani ya udhibiti wa mwanadamu yeyote."

Kwa ujumbe huu rahisi imetolewa 'Zawadi Kwa An-Nadwah'. Katika riwaya hii fupi na ya kusisimua, Hadrat Mirza Ghulam Ahmad anajibu ubishi uliotolewa na Hafidh Muhammad Yusuf kwamba hata wadai wa uongo wa Utume wanaweza kuanzisha misheni yenye mafanikio. Kwa kutumia ukosoaji huu Muhammad Yusuf alitarajia kudhoofisha mafanikio ya Masihi Aliyeahidiwa", Kwa hoja zenye nguvu na zenye hoja Hadrat Mirza Ghulam Ahmad anaichambua tasnifu hii na kufichua dosari zake asili.

na kasoro. Anasema kuwa manabii wa uwongo hawawezi kamwe kufaulu na kwamba kushikilia imani hizo ni ukinzani wa moja kwa moja wa mafundisho ya Uislamu. Badala yake, ushindi wa Mitume wa Mwenyezi Mungu ni muujiza na ishara ya Mwenyezi Mungu inayounga mkono ukweli wao. Wasikilizaji wakuu wa kazi hii walikuwa ni maulamaa wa An-Nadwah ambao waliitwa na Hafiz Muhammad Yusuf kuhukumu ubora wa madai haya yaliyokuwa yakibishana.

Zawadi
Kwa
Nadwa

za
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian,
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi[as]

Nakala hii itapatikana kwa Sh. 1,550/=

Je, Wajua?

Je wajua papa Urban VIII katika mwaka 1633 alimhukumu galileo galilei kifungo cha Maisha katika nyumba yake (kifungo cha nyumbani) kwa muda wote wa Maisha yake kwa kosa la kuamini kuwa jua lipo katikati na dunia inazunguka jua. Miaka takribani alfu moja iliyopita, Quran ilinadi kuwa dunia inazunguka jua.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie
mapenziyamungu36@gmail.com